**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI RA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MBARALI**
**SHULE YA SEKONDARI RUJEWA**

# FOMU YA MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE 2024/2025

SHULE YA SEKONDARI RUJEWA,
S.L.P 133,
**RUJEWA – MBEYA.**
**16/04/2024**

**KUMB.NA.MSS/JI/K.5/19/1/……….**
JINA LA MWANAFUNZI ……………………………………………………………………
ANUANI ……………………………

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA TANO MWAKA 2024/2025</u>**

1. Ninayo furaha kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha tano, Shule ya Sekondari Rujewa Mwaka 2024 katika tahasusi ya **PCM,PCB,CBG,HGL na PMC**, Shule yetu ni ya bweni na ni ya mchanganyiko yaani wavulana na wasichana. Hongera sana kwa kuchaguliwa katika shule hii nakutakia maandlizi mema na safari njema, karibu sana Shule ya Sekondari Rujewa.
2. **MAHALI SHULE ILIPO**
   Shule ya Sekondari **Rujewa** ipo mji wa **Rujewa** katika wilaya ya **Mbarali** mkoa wa **Mbeya**. Kama unatoka Mbeya mjini, panda magari yanayokwenda Rujewa (Pandia stendi ya Nanenane au Uyole) na ukifika stendi Rujewa chukua usafiri hadi shuleni. Wanaotokea Songea, Njombe, Dodoma, Dar es salaam n.k kuja Mbeya shuka kituo kinachoitwa **IGAWA** kisha chukua usafiri ambao unapatikana kwa urahisi kama bajaji na pikipiki. Umbali toka **IGAWA** hadi shuleni ni **KM 1O** na umbali kutoka Rujewa stendi hadi shuleni ni **KM 1.5.**
3. Nauli: Mbeya mjini – Igawa = Tshs 7,000/=. Igawa – Rujewa stendi = Tshs 1,000/=.
4. Hali ya hewa ya Rujewa ni ya joto (Bonde la ufa Usangu) wakati wa mchana na baridi wakati wa usiku.
5. Uaminifu, utii, juhudi, maarifa na nidhamu safi kwa ujumla vitakuwezesha kufanikiwa kitaaluma na kukujengea tabia nzuri na mwenendo mzuri.
6. Unatakiwa kufika shuleni tarehe 01/07/2024, masomo yataanza rasmi tarehe 02/07/2024. Tafadhali unatakiwa kufika shule na michango pamoja na vifaa vyote ulivyoagizwa.

## 1.0 YAFUATAYO NI MAAGIZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA SHULE HII AMBAYO NI MUHIMU UYAFUATE

### 1.1 SARE YA SHULE

#### (A) WAVULANA

(i) Mashati mawili (2) meupe ya mikono mirefu aina ya tetron.

(ii) Suruali mbili (2) rangi ya Dark Blue zenye linda mbili kila pande (celebration). Pia suruali moja nyeusi kwa ajili ya kushindia, ziwe na turn up na zisiwe za kubana (modal).

(iii) Mkanda rangi nyeusi na usiokua na picha wala maandishi au mapambo yoyote.

(iv) Godoro ft 2 ½ x 6.

(v) Tai rangi ya Dark Blue iwe ya wastani (Isiwe ndefu sana wala fupi sana)

(vi) Viatu vya ngozi rangi nyeusi (vya kamba na visiwe vya mchongoko na vyenye visigino vifupi).

(vii) Soksi jozi mbili (2) nyeusi.

(viii) Sweta la rangi ya Dark Blue lenye shingo ya "V".

(ix) T – shirt rangi ya Light Blue (aina ya form six) yenye mchirizi mweusi mikononi na kwenye kora, inapatikana shuleni kwa atakaependa tsh. 12,000/=

(x) Track suit rangi nyeusi (kuanzia mbili) yenye michirizi meupe.

#### (B) WASICHANA

(i) Blauzi mbili (2) nyeupe za mikono mirefu aina ya tetron yasiyo na urembo wowote ule.

(ii) Sketi mbili (2) rangi ya Dark Blue ndefu za linda box kitambaa kigumu (Zifike kwenye kifundo cha mguu)

(iii) Tai rangi ya Dark Blue iwe ya wastani (Isiwe ndefu sana wala fupi sana)

(iv) Godoro ft 2 ½ x 6.

(v) Shamba dress (gauni) mshono solo kuanzia mbili (2) draft rangi ya dark blue ifike kwenye kifundo cha mguu.

(vi) Viatu vya ngozi rangi nyeusi (vya kamba na visiwe vya mchongoko na vyenye visigino vifupi).

(vii) Soksi jozi mbili (2) nyeupe.

(viii) Sweta la rangi ya Dark Blue lenye shingo ya "V".

(ix) Kwa waislamu watashona nusu kanzu nyeupe mbili ambazo ni ndefu kidogo ikiambatana na hijjabu mbili ndefu kidogo.

(x) Track suit rangi nyeusi (kuanzia mbili) yenye michirizi meupe.

Si jukumu la shule kumshonea sare mwanafunzi hivyo basi mzazi/mlezi tunaomba uzingatie maelekezo yaliyotolewa katika ushonaji wa sare hapo juu ili kuepusha usumbufu kwa mwanafunzi.

NB: MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA MAVAZI YA AINA YOYOTE ILE ZAIDI YA SARE ZILIZOTAJWA HAPO JUU

### 1.2 MAHITAJI YA WOTE

(i) Mashuka mawili rangi ya pink na blue bahari.
(ii) Foronya mbili (2) za mito ya rangi ya pink na blue bahari.
(iii) Chandarua cha mbu.
(iv) Blanketi moja jepesi
(v) Sanduku la chuma na kufuri lake

### 2.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Wizara ya Elimu No. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya kusimamia elimu hapa nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:-

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika shughuli mbalimbali ndani na nje ya shule ni muhimu.
iii. Kutimiza/kutekeleza kwa makini maandalio ya jioni (night preparations)
iv. Kuwahi katika kila shughuli ndani na nje ya shule.
v. Kufahamu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako hapa shuleni.
vi. Kutunza usafi wa mwili wako na mazingira ya shule.
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa.
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
ix. Kutunza mali za shule
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye incha kali na dawa bila idhini ya daktari
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

ZINGATIA

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala Kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi Kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum**

toka kwa mkuu wa shule (msiba au ugonjwa)

## 3.0 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE

(i) Wizi
(ii) Utoro wa kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku tisini (90) bila taarifa yoyote ile.
(iii) Kugoma au kuhamasisha migomo
(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi pamoja na jamii kwa ujumla.
(v) Kupigana na wanafunzi wenzake, kumpiga mwalimu au mtu yeyote Yule.
(vi) Kusuka nywele (mwanafunzi anatakiwa kuwa na nywele fupi muda wote).
(vii) Kufuga ndevu.
(viii) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji wa sigara.
(ix) Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa/kuolewa.
(x) Kupata ujauzito kusababisha mimba, au kutoa mimba.
(xi) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo mengineyo yanayovunja sheria za nchi.
(xii) Kutembelea majumba ya starehe pamoja na nyumba za kulala wageni.
(xiii) **Kumiliki simu ya mkononi au laini ya simu na kuvitumia katika mazingira ya shule.**
(xiv) Kumpa mwanafunzi mwenzake ujauzito.
(xv) Kudharau bendera ya Taifa
(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua kama kunywa sumu n.k.
(xvii) Kuharibu mali ya umma kwa kukusudia.

## 4.0 VITU VINGINE MUHIMU AMBAVYO MWANAFUNZI ANATAKIWA KUJA NAVYO ANAPORIPOTI

(i) Mavazi ya michezo (yasiwe ya kubana) kama vile T – shirt (Taifa stars rangi ya blue), raba.
(ii) Ream ya karatasi A4 mbili (2)
(iii) Dissecting Kit kwa wanafunzi waliochaguliwa tahasusi ya PCB na CBG.
(iv) Koti la Maabara (Rangi nyeupe urefu unaozidi magoti) kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.
(vii) Scientific Calculators kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi.
(viii) Vyombo vya kulia chakula yaani sahani, kijiko na kikombe.
(ix) Ndoo ndogo mbili (2).
(x) Daftari kubwa (Counter book) zisizopungua 10 pamoja na mkebe, peni, rula.
(xi) Reki moja (1), jembe moja (1), fagio ya ndani (brush) moja (1), fagio ya nje (chelewa) moja (1) pamoja na panga moja (1).
(xii) Vitabu vya masomo husika katika tahasusi aliochaguliwa mwanafunzi.
(xiii) NAKALA YA HATI YA MATOKEO (**RESULT SLIP**) YA KIDATO CHA NNE.

(XIV) UNASHAURIWA KUJA NA BIMA YA AFYA

## 5.0 ADA NA MICHANGO MUHIMU YA SHULE

(a) Tsh. 65,000/= kwa ajili ya uendeshaji wa shule
(b) Tsh. 5,000/= kwa ajili ya tahadhari (ambayo haitarejeshwa).
(c) Tsh. 5,000/= kwa ajili ya kitambulisho.
(d) Tsh. 5,000/= kwa ajili nembo ya shule.

Michango yote tajwa hapo juu inatakiwa kulipwa benki na mwanafunzi aje na stakabadhi ya malipo (pay in slip). Hakuna pesa ya mwanafunzi itakayopokelewa shuleni. Michango hiyo ilipwe kwenye akaunti namba **61101100001** yenye jina **RUJEWA SECONDARY SCHOOL REVENUE COL** katika benki ya NMB.

**NB: NYUMA YA STAKABADHI YA MALIPO (PAY IN SLIP) YAANDIKWE MAJINA YA MWANAFUNZI NA MCHANGANUO WA MALPO HUSIKA NA KUWASILISHWA SHULENI WAKATI WA KURIPOTI, FEDHA TASLIMU HAZITAPOKELEWA.**

## 6.0 MENGINEYO

### (A) MAANDALIO YA JIONI

(i) Kila mwanafunzi anatakiwa kuhudhuria maandalio ya jioni kwa siku zote za wiki yaani jumatatu mpaka jumapili kuanzia saa 2:00 usiku mpaka saa 4:00 usiku
(ii) Walimu wa zamu watapita kila siku kuangalia mahudhurio ya wanafunzi.

### (B) KUWAHI

(i) Kuwahi katika shughuli za shule kama ratiba za kila siku zilivyopangwa.
(ii) Kuwahi kufika shuleni kwa tarehe zilizopangwa (hasa wakati wa kurudi kutoka likizo)

### (C) SARE YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa katika sare za shule wakati wote wa:-
(i) Masomo darasani
(ii) Kutoka nje ya shule kwa shughuli za kishule
(iii) Kuhudhuria baraza la shule
(iv) Kwenda hospitali
(v) Kazi za mikono (vazi la kazi)
(vi) Michezo (vazi la michezo)
(vii) Kwenda ibadani (kanisani au msikitini)

## (D) MIPAKA YA SHULE

Kila mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mipaka ya shule kama ifuatavyo:-
(i) Kutotoka nje ya mipaka ya shule bila kuwa na kibali cha Mkuu wa shule
(ii) Kutotembela sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalum

- Maabara
- Nyumba za walimu na wafanyakazi wengine
- Ofisi za shule

## (E) TAALUMA

Kutokana na hali ya uhaba wa vitabu hapa shuleni, ni muhimu kwa Mzazi/Mlezi kumnunulia mwanafunzi vitabu husika katika tahasusi aliyochaguliwa kwa kadri atakavyoweza. Baadhi ya vitabu hivyo ni kama vilivyoorodheshwa kwenye jedwali hapo chini:-

| NA | SOMO | JINA LA KITABU |
|---|---|---|
| 1 | CHEMISTRY | - Conceptual Chemistry for class XI and XII by Chand, S.<br>- Advanced Level Inorganic Chemistry by Tanzania Institute of Education<br>- A – level Chemistry 4$^{th}$ Edition by Ramsden, E.M<br>- Advanced Chemistry review paper 1 & 2 |
| 2 | BIOLOGY | - Biological Science 3$^{rd}$ Edition by Taylor<br>- Understanding Biology 4$^{th}$ Edition by Glenn and Tod, S.<br>- Conceptual Biology for class XI and XII by Chand, S.<br>- Advanced Level Biology by Tanzania Institute of Education<br>- Advanced Biology review paper 1 & 2 |
| 3 | PHYSICS | - Conceptual Physics for class XI and XII by Chand, S.<br>- Understanding Physics<br>- Nelkon and Parker Physics<br>- Roger's Physics<br>- Ransden Physics<br>- Advanced Physics review paper 1 & 2 |
| 4 | ADV. MATH | - Tranta Math's<br>- Mathematics for class XI and XII by Chand, S.<br>- Understanding Mathematics<br>- Mathematics volume 1 & 2<br>- Advanced Mathematics review paper 1 & 2 |
| 5 | BASIC APPLIED MATH. | - Basic Applied Mathematics for form 5 & 6<br>- Basic Applied Mathematics review paper 1 & 2 |
| 6 | COMPUTER SCIENCE | -Tanzania Institute of Education<br>-Computer networking; by Ross (2010)<br>-Computer Architecture: By J.P hayes (1998) |

| | | |
|---|---|---|
| | | -Data communication and networking: By Behrouz, A,forouzan (20006) |
| 6 | GENERAL STUDIES | - General Studies for form 5 & 6<br>- General Studies Approach |
| 7 | HISTORY | - The Growth of African Civilization, the Revolutionary Years of West Africa since 1800 by Webster, J.B<br>- How Europe Underdeveloped Africa by Rodney, W<br>- Contemporary Historical Events<br>- A History of Modern Europe 1789 – 1981 by Peacock, H.L<br>- Advanced Learner's History<br>- Mastering Advanced Level History<br>- History review paper 1 & 2 |
| 8 | GEOGRAPHY | - Africa a study of Geography for Advanced students by Pritchard, J.M<br>- Success in Geography Climatology and Soil Science by Msabila, D.T<br>- Physical Geography for Africa by Kamili, Z<br>- Physical Geography by Msabila, D.T<br>- Practical Geography Alive by Kamili, Z<br>- An Integrated Regional Study on Human and Economic Geography (Advanced Level Paper 2) by Msabila, D.T<br>- Geography review paper 1 & 2 |
| 9 | LANGUAGE | - Comprehensive English Grammar New Edition by Archery, N.<br>- Semantics, Phonology and Stylistics by Kadeghe, M.<br>- NOVELS (The Beautiful One Are Not Yet Born by Armal, K., A Man of the People by Achebe, C. etc)<br>- PLAYS (An Enemy of the People by Ibsen, H., I Will Marry When I Want by Ngugi Wa Thiongo etc)<br>- POETRY (Selected Poems)<br>- English review paper 1 & 2 |

## 7.0 FOMU ZIFUATAZO ZIMEAMBATANISHWA NA NI MUHIMU KUZIKAMILISHA

(i) Taarifa ya wazazi/walezi na mwanafunzi
(ii) Kukubali kujiunga na shule
(ii) Kutoshiriki migomo/fujo/makosa ya jinai
(iii) Kukubali kulipa michango
(iv) Fomu ya kupima afya (Medical Examination)

## MWISHO:-

Shule hii inathamini umoja, amani na juhudi katika masomo na kazi za nje. Nidhamu safi ni msingi wa mafanikio ya kila binadamu hivyo kila atakayekubali kujiunga na shule hii atatakiwa kuzingatia maelekezo hayo. Sheria za Shule zimeambatanishwa, sizome kwa makini na uwe tayari kuzifuata.

KARIBU SANA RUJEWA SEKONDARI

……………………………..
LAZARO A. MALAMBUGI
MKUUU WA SHULE
0754 – 213588

NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahutihuti hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:

- Mkuu wa shule 0754 213588
- Makamu mkuu wa shule 0764 846025/0756729078
- Mwandamizi Taaluma 0764961940
- Mwandamizi malezi 0755764593

.                                   KIAMBATA ‘A’

## TAARIFA YA WAZAZI/WALEZI NA MWANAFUNZI

### SEHEMU A: TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI (Ijazwe na Mwanafunzi)

Jina kamili (Kama lilivyo kwenye result slip) ………………………………………………………

Tarehe ya kuzaliwa ……………………… Kabila ………………… Dini/Dhehebu…………………

Tahasusi (Combination) uliyochaguliwa ……………………… Shule utokayo …………………

Mahali unapoishi ……………………………… Mkoa …………………… Wilaya …………………….

Anwani (S.L.P) ……………………..

### SEHEMU B: TAARIFA ZA WAZAZI/WALEZI

Jina la baba mzazi/mlezi ………………………………………Kazi yake ……………………………

Jina la baba mama/mlezi ………………………………………Kazi yake …………………………..

Mahali Mzazi/Mlezi anapoishi ……………………. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………

Namba ya simu ya Mzazi/Mlezi …………………. Mahali nitakapokua nakwenda wakati

wa likizo ni kwa (mtaje) ……………………. Wapi …………………… Simu……………………

Nathibitisha kuwa taarifa nilizotoa hapo juu ni za kweli na sahihi

Sahihi ya Mwanafunzi …………………………………. Tarehe ……………………………………….

## KIAMBATA 'B'

## KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Mimi …………………………………. nimesoma kwa makini maagizo yote na ninatambua kuwa kuchaguliwa kwangu kujiunga na Shule ya Sekondari Rujewa ni bahati na zawadi kubwa kwa kuwa wengi wamekosa nafasi si kwa kuwa wameshindwa ila kwa sababu nafasi ni chache.

Hivyo nakubali kujiunga Rujewa Sekondari, nitatii na kufuata sheria na taratibu zote za Shule. Nitajitahidi kufanya/kusoma kwa juhudi na maarifa na nitajitahidi kushirikana na wenzangu kweli daima.

Nitalinda hadhi/heshima ya Shule ya Sekondari Rujewa na nitashirikiana na wenzangu kujenga misingi na historia nzuri ya shule.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………… Tarehe ………………………………………….

Mimi Mzazi/Mlezi ……………………... nimeshudia mtoto wangu ………………………………
akikubali kwa hiari kujiunga na shule ya Rujewa Sekondari, hivyo ninaamini mtajitahidi kumfunza na kumlea vizuri. Mimi pia naahidi kushirikiana nanyi kikamilifu katika kulea mtoto wangu kwa kila hali.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi

## KIAMBATA 'C'

## KUTOSHIRIKI MIGOMO/FUJO/MAKOSA YA JINAI
(Ijazwe na Mwanafunzi mwenyewe)

Mimi ………………………………………………. Umri ……………………. Jinsi (Me) ☐ (Ke) ☐

naahidi kwamba nitakua mwadilifu, mwaminifu na kwamba sitashirki, kusababisha

wala kuchochea mgomo kwa namna yeyote ile na nitatoa taarifa kwa utawala pale nitakapoona viashiria vya mgomo, fujo au uvunjifu wa amani shuleni. Aidha naahidi kwamba hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yangu ikiwa pamoja na kusimamishwa au kufukuzwa shule iwapo nitabainika kuwa nimeshiriki makosa yalioainishwa katika kifungu hiki.

Sahihi ya mwanafunzi ……………………………… Tarehe

## KIAMBATA 'D'

## KUKUBALI KULIPA ADA NA MICHANGO MENGINE

**(Ijazwe na Mzazi/Mlezi)**

Mimi ……………………………… ambaye ni …………………. Wa mwanafunzi huyu. Nimesoma kwa makini maelekezo pamoja na sheria za shule katika fomu ya kujiunga na nipo tayari ajiunge na shule hii. Naahidi kumtolea mtoto wangu ada, michango na mahitaji mengine ili aweze kupata elimu yake vizuri katika shule hii. Aidha nitasaidiana na walimu/walezi wa shule katika kumlea mtoto wangu katika maadili mema na kuitikia wito wa kufika shuleni pale nitakapohitajika. Aidha taarifa zote za maendeleo ya kitaaluma ya mtoto wangu zitanikifika zikitumwa kwa:-

Jina (Mzazi/Mlezi) ……………………………………………….. S.L.P ………………………………..

Namba ya simu …………………….

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………  Tarehe …………………………………………

Picha na namba za simu za ndugu watakaoweza kumtembelea mwanafunzi akiwa shuleni

1. ………………………………………… Simu …………………………………………………
2. ………………………………………. Simu ………………………………………………….
3. ………………………………………… Simu ………………………………………………….
4. ………………………………………. Simu ………………………………………………….

| 1. | 2. | 3. | 4. |
|---|---|---|---|
| Weka picha hapa kulingna na namba hapo juu | Weka picha hapa kulingana na namba hapo juu | Weka picha hapa kulingana na namba hapo juu | Weka picha hapa kulingana na namba hapo juu |

.                KIAMBATA ‘E’

## FOMU YA KUPIMA AFYA (MEDICAL EXAMINATION)

## FOR MEDICAL EXAMINATION

To be completed by medical officer in a respect to all form of entrants.

Student’s full name ........................................... Age…………Years……… Sex……………

Blood count (Red and White)…………………………………………………………………………………..

Stool examination………..................................................................................

Urine analysis……………………………………………………...............................................

Syphilis test…………………………………………………………….…….…………………………………..

Eye test……………………………………………………………………….....................................

T.B test………………………………………………………………….........................................

Ears………………………………………………………..................................................

Chest…………………………………………………………………………………………………………….

Spleen…………………………………………………………………………………………………………..

Abdomen…………………………………………………………………..…………………………………….

**ADDITIONAL INFORMATION** e.g. physical or chronically family diseases etc

……………………………………………………………………..…………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………..

I certify that the above named student is fit to peruse studies

Name……………………………………………Station…………………………………

Signature………………………Date……………………………………  Designation……………………….

**NOTE**: Medical officer at the time of examination the individual for any aliments you note.

**STUDENTS:**

You must bring this complete form when you come to school, no student may enroll without certificate of physical fitness.